

**CHA.KI.TA**  
**Chama cha Kiswahili cha Taifa-Kenya**  
**SLP 66872-00800**  
**NAIROBI**

**ARIFA YA KONGAMANO**

Chama cha Kiswahili cha Taifa (CHAKITA-Kenya) kitakuwa na Kongamano mnamo mwezi wa Agosti 23-24, 2012 katika Chuo Kikuu cha Kenyatta, mjini Nairobi.

**MADA KUU: KISWAHILI, UWIANO, UTANGAMANO NA MAENDELEO**

**Malengo:**

- Kudahili mchango wa Kiswahili katika kuleta na kudumisha uwiano, utangamano na umoja.
- Kujadili nafasi ya lugha ya Kiswahili barani Afrika na kwingineko katika kuleta maendeleo katika nyanja mbalimbali.
- Kutathmini mchango wa vyombo vya habari katika uendelezaji wa lugha ya Kiswahili.
- Kuchunguza swala la lugha katika maendeleo ya elimu, utamaduni, demokrasia, sayansi na teknolojia.

**Mada Ndogo:**

1. Kiswahili Ndani na Nje ya Afrika Mashariki
2. Kiswahili, Sayansi na Teknolojia
3. Kiswahili na Vyombo vya Habari
4. Kiswahili na Utekelezaji wa Rajua za Taifa
5. Kiswahili, Uwiano na Utangamano
6. Kiswahili, Katiba na Elimu ya Jamii
7. Kiswahili na Uchapishaji wa Kiakademia
8. Lugha katika Fasihi
9. Kiswahili na Uondoaji wa Umaskini
10. Kiswahili na Uzalishaji Vyakula
11. Kiswahili na Demokrasia
12. Kiswahili na Masuala ya Afya
13. Kiswahili na Usuluhishaji wa Migogoro

**Zingatia Yafuatayo:**

1. Lugha ya kongamano itakuwa Kiswahili.
2. Tafadhali tuma mada na ikisiri isiyozidi maneno 300 kwa:  
Kamati Andalizi  
Kongamano la Kiswahili 2012  
SLP 43844-00100  
Nairobi

AU

Barua pepe: Prof. Kimani Njogu: [kimani.njogu@gmail.com](mailto:kimani.njogu@gmail.com); Dkt. Pamela Ngugi [muhadiap@yahoo.com](mailto:muhadiap@yahoo.com) na Prof. Clara Momanyi: [clamona@yahoo.com](mailto:clamona@yahoo.com)

Tarehe ya mwisho ya kupokea ikisiri ni Mei 15, 2012.

3. Wajumbe watawasili tarehe 22/08/2012 na Kongamano litaanza rasmi tarehe 23/8/2012.
4. Wajumbe watagharimia usafiri, malazi na chakula. Chama kitagharimia chakula cha mchana na chai.
5. Ada za kongamano ni kama ifuatavyo:
  - (a) Ada ya wanachama: Kshs. 2,000/=
  - (b) Ada ya wasio wanachama: Kshs. 3,000/=
  - (c) Ada ya wale watokao nje ya Afrika: Dola 50 za Marekani
  - (d) Ada ya wanafunzi wa shahada za juu: Kshs. 2,000/=
  - (e) Ada ya wanafunzi wa shahada ya kwanza: Kshs. 500/=